



## **HOTUBA YA**

### **WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB.) KWENYE UZINDUZI WA SIKU YA LISHE KITAIFA TAREHE 07 AUGOSTI 2020 NYERERE SQUARE –DODOMA**

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Suleiman Jaffo;  
Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Dkt. Binilith Mahenge;  
Katibu Mkuu Wizara ya Afya;  
Mganga Mkuu wa Mkoa Dodoma;  
Mkurugenzi Idara ya Huduma Kinga;  
Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe;  
Mganga Mkuu Wilaya Dodoma;  
Wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa;  
Wadau wa Maendeleo na Asasi za Kiraia;  
Wawakilishi wa Idara na Taasisi za Serikali;  
Ndugu Wageni Waalikwa, Waandishi wa habari na wadau wote wa  
Lishe.**

#### **Mabibi na Mabwana;**

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa Jijini Dodoma kwa ajili ya uzinduzi rasmi wa Siku ya Lishe nchini. Aidha, nitumie nafasi hii kuushukuru uongozi mzima wa Wizara ninayoiongoza, kwa kusimamia uratibu wa maandalizi ya maadhimisho haya; Ofisi ya Waziri Mkuu

pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ushiriki wao katika utekelezaji wa masuala ya lishe katika ngazi mbalimbali.

Pia, ninapenda kuwapongeza sana waratibu wa mkutano huu, Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania pamoja na Kitengo cha Huduma za Lishe kwa kufanikisha maandalizi na kuweza kuwaleta wadau wote wa lishe nchini pamoja.

**Mabibi na Mabwana;**

Tumekusanyika hapa siku ya leo kwa ajili ya kuzindua rasmi kwa mara ya kwanza maadhimisho ya Siku ya Lishe Kitaifa. Siku hii itakua ikiadhimishwa kila ifikapo tarehe **7 Agosti** ya kila mwaka. Maadhimisho haya ya Kitaifa yanalenga kuwaleta kwa pamoja wananchi ili kutambua na kufahamu umuhimu wa Lishe bora na kuwa chachu ya mabadiliko katika ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha.

Aidha, Uzinduzi huu pamoja na maadhimisho yatakayoendelea miaka mingine yatumika katika kuhamasisha utekelezaji wa shughuli za lishe katika ngazi za Mikoa na Halmashauri ili kutatua matatizo ya lishe yaliyopo katika maeneo yao husika; kuelimisha na kuhamasisha umma wa watanzania kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa kutumia jumbe mbalimbali; kufanya tathmini ya hali ya lishe na kutoa ushauri kwa wananchi.

**Mabibi na Mabwana;**

Serikali inatambua kuwa lishe bora ni msingi wa maendeleo ya Taifa letu, na ni moja ya eneo la kipaumbele cha kimaendeleo. Uwepo wetu sote katika uzinduzi huu unaendelea kuonesha umuhimu wa kuimarisha ushiriki wa kila sekta, kila mdau ikiwemo sekta binafsi kwa nafasi yake, na wananchi kwa ujumla katika kupambana na aina zote

za utapiamlo. Maadhimisho haya yaletе chachu katika kujenga Taifa lenye watu wenye afya njema na ufahamu mzuri wenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo za kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na kazi za viwandani na maofisini. Tukiwa na jamii yenye lishe bora, ni dhahiri kuwa tutakuwa tumefanikiwa kupambana na maradhi, ujinga na umaskini na hatimaye Taifa letu kuwa nchi ya Uchumi wa Viwanda kama ilivyodhamiriwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**.

Kauli mbiu ya maadhimisho haya kwa mwaka huu ni “***Mlo kamili kwenye jamii yetu unawezekana***”. Kauli mbiu hii inalenga kutukumbusha umuhimu wa kula mlo kamili katika kila mlo ili kuupatia mwili virutubishi muhimu kwa lishe na afya bora. Ikumbukwe kuwa mlo kamili unatokana na ulaji wa vyakula mchanganyiko kutoka katika makundi matano ya vyakula vinavyopatikana katika jamii yetu.

Mlo kamili unajengwa na vyakula vinavyotokana na makundi matano (5) ya vyakula, ambapo kundi la **kwanza** linahusisha vyakula vyenye asili ya nafaka, mizizi na ndizi mbichi; kundi la **pili** linahusisha vyakula vyenye asili ya wanyama na mikunde; kundi la **tatu** ni mboga mboga; kundi la **nne** ni matunda; na kundi la **tano** ni mafuta, sukari na asali. Nimearifiwa kuwa leo katika maadhimisho haya, tutapata fursa ya kuona jinsi ya kuandaa mlo kamili, kwa kutumia vyakula vinavyopatikana hapa Jijini Dodoma.

### **Mabibi na Mabwana,**

utapiamlo ni tatizo la muda mrefu, na nchi yetu imepiga hatua katika kupunguza viwango vya utapiamlo katika jamii, hususan miongoni mwa watoto wadogo, vijana balehe na akina mama walio katika umri

wa kuzaa. Utafiti wa kwanza mkubwa kuhusu hali ya lishe nchini ulifanyika kati ya mwaka 1964 na 1967 katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Pwani na wilaya ya Karagwe na ulibaini kuwa, kati ya asilimia 40-66 ya watoto waliokuwa na umri chini ya miaka mitano walikua na utapiamlo.

Kwa miaka ya karibuni Serikali imeongeza juhudi za kupambana na tatizo la utapiamlo nchini kwa kushirikiana na wadau wetu wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Juhudi mbalimbali zilizofanyika ni pamoja na:

- Kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Afua za Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan- NMNAP 2016/17-2021/22), ambao umezinduliwa na kuanza kutekelezwa mwaka 2016.
- Kuanzishwa kwa kada ya Maafisa Lishe katika Mikoa na Halmashauri zote nchini mwaka 2012 pamoja na Waratibu wa Lishe katika sekta zinazotekeleza huduma za Lishe.
- Kuanzishwa kwa Kamati Tendaji Jumuishi ya Lishe ngazi ya Taifa inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Kamati Tendaji Jumuishi za Mikoa na Halmashauri. zinazosimamia masuala ya Lishe katika ngazi za Taifa, Mikoa na Halmashauri.
- Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imeazimia na inaendelea kutekeleza afua za lishe zenye matokeo makubwa kama vile: utoaji wa vidonge vya Madini Chuma na Asidi ya Foliki kwa wajawazito, utoaji wa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo, uongezaji wa virutubishi vya madini na vitamin kwenye chakula, matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto wa chini ya miaka mitano,

utoaji elimu na huduma za Lishe kwa wanawake, vijana balehe, watoto wachanga na wadogo, elimu ya ulaji vyakula mchanganyiko na mtindo bora wa maisha kwa wanajamii wote.

- Kufanya maboresho na kupitia sera na miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa afua muhimu za Lishe nchini.
- Katika kuongeza kasi ya kupambana na utapiamlo nchini, Serikali ya Awamu ya Tano ilitoa Mwongozo kwenye Bajeti ya mwaka 2017/18 wa kutenga kiasi cha shilingi 1000 kwa ajili ya masuala ya lishe kwa kila mtoto wa umri chini ya miaka mitano. Kiwango ambacho kitaendelea kuongezwa taratibu katika bajeti zijazo hadi kufikia kiasi cha dola 8.5 sawa na shilingi 18,000 kwa kila mtoto kama lilivyoshauri na Jopo la wataalamu wa Benki ya Dunia na wa masuala ya Afya na Uchumi Ulimwenguni.

Hivyo, kutokana na juhudi hizo tumeshuhudia kuboreka kwa hali ya lishe kwa kutumia viashiria mbalimbali. Kulingana na utafiti wa hali ya lishe nchini uliofanyika mwaka 2018, matokeo yake kuonesha:

- Udumavu umepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018; na
- Upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa umepungua kutoka asilimia 45 mwaka 2010 mpaka asilimia 29 mwaka 2018.
- Pia tumeendelea kuwa na viwango vidogo vya watoto wenye ukondefu ambapo mwaka 2014 ulikuwa asilimia 4.5 na kwa utafiti wa mwaka 2018 ni asilimia 3.5

Hata hivyo, takwimu hizo zimeonesha bado tuna changamoto ya ongezeko la uzito uliozidi na kiribatumbo kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa kutoka asilimia 29.7 mwaka 2014 mpaka asilimia 31.7

mwaka 2018. Aidha, viwango vya ulishaji wa wa vyakula vya nyongeza miongoni mwa watoto walio na umri wa miezi 6 hadi 23 bado viko chini ambapo kwa mwaka 2018 ni asilimia 33 tuu ya watoto hao walipata vyakula vya nyongeza ipasavyo, yaani milo kutoka kwenye makundi yote yanayotakiwa na idadi ya milo inayopaswa kuliwa.

Ni dhahiri kuwa, matatizo ya lishe nchini yanatokana na jamii kutokuzingatia ulaji unaofaa wa vyakula kutoka katika makundi hayo matano kama inavyoshauriwa na wataalaam wa lishe.

### **Mabibi na Mabwana;**

Nitumie fursa hii pia kuainisha tatizo la ulaji mashuleni, ambapo tunashuhudia wanafunzi kuendelea kutumia vyakula visivyo na virutubishi vya kutosha ambavyo huuzwa kwa wingi katika maeneo ya Shule. Hivyo, natoa rai kwa viongozi na wawakilishi wa kisekta mlioko katika maadhimisho haya, kusimamia namna ya ulaji unaofaa mashuleni ikiwemo ulaji wa mbogamboga na matunda pamoja na unywaji wa maziwa. Kulingana na taarifa za shirika la Afya Duniani, mtu anahitaji kunywa nusu lita ya maziwa kwa siku, lakini kwa Tanzania matumizi ni lita 40 tu kwa mwaka kwa mtu mmoja. Ni vyema sasa tukazitaka shule zote nchini kuhamasisha juu ya upatikanaji na matumizi ya maziwa katika maeneo ya shule pamoja na vyakula vingine mchanganyiko.

Katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na mwongozo sahihi wa uandaaji wa vyakula cha nyongeza kwa watoto, nimetaarifiwa kuwa, Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kupitia ufadhili wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), itafanya utafiti wenye lengo la kutengeneza mchanganyiko wa chakula cha nyongeza chenye

virutubishi vya kutosha. Aidha, mchanganyiko huu utakuwa ndio kigezo elekezi katika viwango vya uzalishaji wa ndani kwa wajasiriamali na wazalishaji wa chakula hicho.

### **Mabibi na Mabwana;**

Ninaamini kuwa uwepo wa maadhimisho ya siku ya lishe Kitaifa itakuwa ni chachu katika kubadili tabia za wananchi kuhusu ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha ili kuboresha afya na lishe yao.

Baada ya kusema hayo napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote wa lishe ikiwa ni pamoja na watumishi wenzangu wa Wizara, Idara na Taasisi za Umma, Asasi za Kiraia, Wadau wa Maendeleo, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa kwa kuendeleza huduma za lishe hapa nchini. Aidha, ni heshima nyingine kwangu binafsi kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa namna ya pekee Waandishi wa Habari kwa juhudi zenu za kuuelimisha umma wa Watanzania kuhusu masuala ya afya, Chakula na lishe na kutoa elimu sahihi. Hivyo, ninatamka rasmi kwamba kila ifikapo **tarehe 7 ya mwezi wa Nane ya kila mwaka itakua ni siku ya Lishe Kitaifa na itaadhimishwa katika ngazi zote kuanzia Taifa, Mkoa, Halmashauri na hata Vijiji.**

**Asanteni Sana kwa kunisikiliza!!!**